

## MKATABA WA UPANGISHAJI

MAKUBALIANO HAYA YAMEFANYIKA siku ya tarehe .....<sup>01</sup>..... ya mwezi wa .....<sup>07</sup>.....  
..... mwaka 2023

### BAINA YA

Ndugu **OTTO P. LEBBA** Mkoa wa DODOMA, Wilaya ya CHEMBA, Kata ya LALTA, Kijiji cha MAGAMBUA, Kitongoji cha MENDUSEE, Nyumba Na. 52, S.L.P 830. Ambaye ndani ya Mkataba huu atakuwa anatajwa kama **MPANGISHAJI**.

### NA KAMPUNI YA

**FUXING RESOURCES LIMITED** Region MWANZA, District NYAMAGANA, Ward NYAMAGANA, Postal Code 33101, Street NYAMAGANA CAPRI POINT, Road NYAMAGANA, Plot Number 20X, Block Number 20X, House Number NIL. Ambaye ndani ya Mkataba huu atakuwa anatajwa kama **MPANGAJI**.

### KWA KUWA:-

- a) **MPANGISHAJI** ndiye, na ataendelea kuwa mmiliki halali wa nyumba iliyopo Magambua Chemba, nyumba ambayo ndani ya Mkataba huu inatajwa kama sehemu ya Makazi.
- b) Na kwamba **MPANGISHAJI** ana hiari, kwa kuzingatia kufuatwa kwa masharti yanayoainishwa kwenye Mkataba huu, ya kumpangisha **MPANGAJI** nyumba kwa ajili ya makazi nashughuli zao binafsi.
- c) Na kuwa **MPANGAJI**, kwa hiari yake yuko tayari kupanga nyumba hiyo pangishwa kwa kufuata, na bila kuvunja masharti yanayoainishwa katika Mkataba huu;

### WAHUSIKA WA MKATABA HUU WANAKUBALIANA YAFUATAYO:

- a) **KWAMBA**, kwa Malipo ya kodi inayoainishwa katika Mkataba huu, na kulingana na masharti ya upangaji kama yanavyoainishwa katika Mkataba huu. **MPANGISHAJI** anapangisha nyumba kwa **MPANGAJI**;
- b) **NA KWAMBA MPANGAJI** Mkataba huu utakuwa ni muda miaka mitatu (3) na atalipa shilingi **700,000/=** (Laki saba) kwa kila mwezi kwa **MPANGAJI**, Malipo ambayo yatafanyika kila miezi Sita kwa kiwango cha shilingi **4,200,000/=** (Shilingi Milioni nne na laki mbili tu) kwa miezi Sita sita.
- c) **NA KWAMBA** Mkataba huu umeanza kutumika siku ya tarehe ..... mwezi wa .....mwaka **2023** ambapo **MPANGAJI** ataruhusiwa kutumia nyumba kwa ajili ya makazi na shughuli binafsi tu

### KWA MASHARTI YAFUATAYO:

- A. Endapo
  - i. Katika kipindi cha upangaji kodi haitokua imelipwa kwa muda wa siku ishirini na moja na /au **MPANGAJI**, bila sababu ya Msingi, akashindwa kuzingatia masharti muhimu ya upangishaji, katika Mkataba huu, Itakuwa ni halali kwa mpangishaji, kutwaa Nyumba yake;
- B. Taarifa (NOTICE) inayohusiana upangaji katika Mkataba huu itakuwa ni kwa ajili ya maandishi;
- C. Mkataba huu unaweza ukarefushwa kulingana makubaliano wa wahusika wote wawili. Katika kipindi chote cha kupitia upya na kurefushwa kwake. Kiasi cha kodi kitajadiliwa upya kulingana na mazingira ya wakati huo.
- D. **MPANGAJI** anaweza akavunja Mkataba kabla ya kumaliza kwa kipindi chake. Baada ya kutoa taarifa ya siku 30 kwa **MPANGISHAJI** lakini kwa hali yoyote uvunjaji wa Mkataba ndani ya kifungu hiki hakiruhusu kurudishwa kwa **KODI** itakayokua imeshalipwa.

**KWA MASHARTI HAYO, MPANGAJI ANAKUBALI YAFUATAYO:**

1. Kulipa **KODI** kwa kiasi kinachotajwa katika mkataba huu.
2. Kwa wakati wote, kuweka Chumba katika hali bora, na usafi kwa matumizi yaliyo kusudiwa.
3. Kuruhusu **MPANGISHAJI** au mtu yeyote kwa niaba yake, kuingia na kufanya matengenezo au ukaguzi unaohusiana na ubora wa Nyumba.
4. Kutofanya upanuzi, au kubadilisha sehemu yoyote ya Nyumba bila ridhaa ya **MPANGISHAJI**;
5. Kutumia nyumba hiyo kwa madhumuni ya makazi na shughuli binafsi kama waliyokubaliana na **MPANGISHAJI**;
6. Kwamba **MPANGAJI** atawajibika kwa uharibifu wa makusudi au uzembe, katika nyumba hiyo
7. Wakati Mkataba utakapofikia ukingoni, na kurefushwa kwake **MPANGAJI** atakabidhi nyumba ikiwa katika hali nzuri

**NA MPANGISHAJI ANAKUBALI YAFUATAYO:**

1. Kuhakikisha kwamba **MPANGAJI** hatopata usumbufu wowote, na kwamba baada ya **MPANGAJI** kulipa **KODI** na kutimiza masharti yote ya **UPANGAJI**, **MPANGAJI** atakuwa huru kutumia nyumba hiyo kwa ajili ya madhumuni yanayoainishwa katika Mkataba huu bila ya vikwazo vyovyote ambavyo ni kinyume na Mkataba.
2. Kufanyia matengenezo nyumba na kuhakikisha kwamba wakati wote iko katika hali nzuri kwa ajili ya makazi na shughuli binafsi pale ambapo hali itayopelekea kuhitajika kwa matengenezo haitokuwa ni kwa ajili ya matendo ya **MPANGAJI**, kwa makusudi au uzembe yatakayosababisha uharibifu:
3. Kulipa Malipo yote katika mamlaka husika, Malipo ambayo **MPANGAJI** hajatajwa kuhusika nayo katika Mkataba huu.

**NA INASHUHUDIWA** kwamba wahusika katika Mkataba huu wameingia Mkataba huu siku hii kama inavyo onekana hapo chini.

**SAINI YA MPANGISHAJI**

TAREHE 01/07/2023

**SAINI YA MPANGAJI**

TAREHE 01/07/2023

**MBELE YA M/KITI WA KIJJI/KITONGOJI**

Halmashaari  
**HALMASHAURI YA KIJJI  
CHUMBA**

TAREHE 01/07/2023

**SAINI YA WAKILI/MWANASHERIA**

PAK

PAK

